
jarida la kifasihi la kila mwezi

# NGURUMO ya mwandishi

TOLEO LA XXVIII
JANUARI MMXXIV



## Ukishindwa Kuona, Basi Chungulia...

## YALIYOMO

**TAHARIRI**— Ukishindwa kuona, basi chungulia—Uk 02

**MWANDISHI WETU**— Hussein B. Mwinshehe — Uk 03

**New In Town:** USIKU WA DENI**—** uk 04

**PITIO LA VITABU**— Gamba la Nyoka (Ikisiri) 8—Uk 06

**MAKALA— SAIKOLOJIA**: Usiwe Chanzo cha Matatizo Yako —Uk 06 na 07

**RIWAYA:** Nilimuua Dada Niolewe Na Shemeji '13'— uk 08 na 09

**MIAMBA WA AFRIKA:** Muammar Gaddafi '03'— Uk 10

**Sako kwa Bako– Eva Mrema: Ku ngwi Mpaka Kwenye Vitabu—**Uk 11

**RIWAYA:** —Kisasi cha Hisia '04'—Uk 12 na 13

**RIWAYA—** Cronoc 7 '10'**-** Uk 14 na 15

**YA KALE NI DHAHABU**: — Alibaba na Wezi 40 '7'- Uk 16

**HABARI:** Wazo La Mwafrika – Uk 17

**SHUBAKA LA VITABU:** Zijue maktaba 10 bora duniani '4'—Uk 18

**KITABU NILICHOSOMA:** I Can, I Must, I Can — Uk 19

**MATANGAZO: -** Uk20

**MALENGA WA KILEO —** Uk 21

**HABARI PICHA: -** Uk 22

**KUTOKA MAKTABA:** Miaka 62 ya Uhuru : Vituko Vya Uhuru**- '3'-**Uk 23

**ELIMU JAMII:** Hakuna Mwanafunzzi Anayependa Kufeli— Uk 24 na 25

**NGURUMO YA MWANDISHI**

**WASILIANA NASI**
**0766 974 865 AU 0627160016**
**WhatsApp: +255 766974865**

## TAHARIRI: Ukishindwa Kuona, Basi Chungulia

Salaam kwako,

Najua, umeuanza Mwaka Mpya kwa furaha kubwa… hayo mengine ya ada za shule ni matatizo madogo madogo ya maisha yanayotokana na utamaduni wetu wa kutokujipanga mapema kwa jambo ambalo twajua kuwa lipo kila mwaka.

Napenda tu kukwambia kuwa maisha yanaendelea hivyo usimfanyie mtu ubaya tuwapo katika hii safari iitwayo 'maisha' maana wa kukuzika humjui. Mengi yametukia, ndugu zetu wengi tumewapoteza hususani kule Manyara, Hanang. Mungu awarehemu wote waliopoteza maisha kwa janga lile.

Sasa tupo toleo la 28, *'Ukishindwa kuona, basi hungulia'*. Ngurumo ya Mwandishi tunakushukuruni sana ninyi nyote mlioweza kutuchangia chochote kwa ajili ya kazi ngumu ya uandalizi wa jarida hili. Mungu akubarikini sana na awaongezee palipopungua. Pia tunakushukuruni ninyi mnaoweka matangazo yenu kwa gharama elekezi, mbarikiwe na Bwana.

Sisi twakutakieni heri sana ya mwaka huu mpya. Tunapenda tu kukuambieni kuwa pale ulipokosea mwaka jana, hakikisha mwaka huu unavuka ili upige hatua mpya katika maisha. Tunahitaji kukua! Kukua siyo kuongezeka urefu au kuongeza namba ya umri wako. Kukua ni kuwa na uwezo mkubwa wa kufikiri ijapokuwa unaendana na hayo niliyoyataja hapo juu.

Hakikisha unapiga hatua moja mbele kutoka ile ya awali ambayo ama ilikukwamisha au ilikudumaza. 2024 ukawe mwaka wako wa kutenda muujiza. Sisi hatuna mengi tunakwambia tu kuwa ukishindwa kuona, basi chungulia. Maana hata ukichungulia utaona.

Hili ni jarida letu sote, yaani mimi na wewe, basi njoo, tuandike, njoo, tupige *soga* za vitabu na fasihi hapa. Ewe mwandishi *'mkubwa'*, njoo ili wadogo wajifunze kutoka kwako nawe unayejiita *'mdogo'* njoo ili wakubwa na hadhira wakufahamu. Tuletee hadithi fupi, mashairi, njoo ujitangaze juu ya kazi zako za kifasihi, tuletee chambuzi zako za vitabu na kadhalika.

Nimekaa hapa nakusubiri…

**Richard R. Mwambe (Amata)**
**Iringa—Tanzania.**
**30/1/2024**

# MWANDISHI WETU: HUSSEIN B. MWINSHEHE

**USIKIAPO 'Tungo Tata Kingdom' si mwingine bali ni kijana machachari mwenye 'ghani andishi' yake mari-dhawa. Katika toleo hili, Ngurumo ya Mwandishi imemfikia na inamleta kwenu…**

Nimezaliwa Kinondoni Dar es salaam July 31,1993. Ni mtoto wa 5 Kwa baba na wa 4 kwa mama. Baba Mluguru wa Matombo Morogoro na Mama ni Mkwele wa Msoga, Pwani. Elimu yangu Kidato Cha Nne. Shule ya Msingi nimesoma Tambuu huko Matombo. Shule ya Sekondari nimesoma Kigamboni/Minazini Dar Es Salaam. *(Utata jina langu na la Babu nililoitwa Shule ya Msingi na sekondari ni tofauti lakini wote ni Babu Zangu wa kweli.)*
Shule ya Msingi niliitwa HUSSEIN B. MWINSHEHE sekondari niliitwa SHABANI B. MWINCHANDE. Sikuwahi kupata Malezi ya Pamoja ya wazazi wangu kwakuwa waliachana punde tu nilipozaliwa.

Mtu wa kwanza kugundua kipaji changu cha uandishi ni baba yangu, ila alinitabiria kuwa karani kwakuwa aliniona napenda sana kuandika. Maisha yangu yalibadilika ghafla baada ya baba kufariki ukatokea ugomvi mkubwa wa mirathi uliopelekea niwe mtoto wa kitaa nikiwa kidato cha kwanza. Ndicho chazo cha kubadilishiwa shule na kutumia jina la babu na la mtoto wake aliyepaswa asome hapo.

Shule ya kwanza kusoma sekondari ni ya Jeshi, Kigamboni Sec. school na huo ndio ulikuwa msaada pekee niliopewa na Babu yangu kipenzi MWINCHANDE ulionifan-ya walau nifike hiko kidato cha nne japo kwa *mbinde!* Maisha yangu nimekua, ni-kashuhudia utata mwingi sana na nimeishi sana Tandale - Uwanja wa Fisi. Utata wa mapito yangu ndo uliopelekea tungo zangu kuwa na mtindo wa kipekee.

Kwakuwa napenda sana amani na imani isiyo na ubaguzi, imepelekea tungo zangu kuwa na mlengo wa imani ingawa kwa mtindo wa utata.

Mashairi nilianza kuyapenda toka shule! Na shairi lililonifanya nitamani kuandika mashairi ni lile la 'KAMA UNATAKA MALI' au wengi huliita 'Karudi Baba Mmoja'. Tungo zangu zimeegama zaidi kwenye jamii hasa ya kitaa na napenda kutumia lugha ya kihuni kwasababu wahuni ndio Jamii iliyonipokea baada ya kutengwa na kaka utotoni kwa sababu ya mirathi.

Huwa napenda kuandika kwa imani na kuvaa hisia za kila mhusika wangu. Nimejiita Mtoto wa Beka kwa sababu ndio jina pekee lisilowahi kubatilika kwenye maisha yangu. Tungo zangu zimeegama sana kuun-ganisha Jamii ya uswazi na ushuani. Na najivunia sana kuwa mtoto wa kitaa kwakuwa nimejifunza mengi ambayo kwa mtu aliyepata malezi bora hawezi kuyajua.

Mpaka sasa nina vitabu vinne vya riwaya
1 - Wanawake ni Wauaji? 2 - German Machine
3 - Singeli Kitaa
4 - Mitaa na Polisi
Na kimoja Cha tenzi.
1 - Je, wanawake ni Wauaji?

Vyote vinapatikana dukani kwetu Tungo Tata Bookshop Manzese, Kona ya Ri-waya Kinondoni, Morogoro Kwa Markus Mpangala, Ubungo fly over.

Pia Nina softicopy vitabu 4; 1 - Mfuasi
2 - Kitanzi Cha Huba
3 - Ndoa Yangu
4 - The Question mark

***RM.***

Penda kusoma vitabu

www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Faida za kusoma vitabu:

- Msisimko wa Akili
- Kupunguza Msongo wa Mawazo
- Kuongeza Ujuzi wa mambo mbalimbali
- Kuongeza Msamiati
- Huboresha Uwezo wa Ku-kumbuka
- Hukupa Uwezo Mkubwa wa kuchambua na kufikiri
- Huboresha Mtazamo na Umakini



## NEW IN TOWN :

## USIKU WA DENI— Gwamaka Mwamasage

Siku chache kabla ya kufanyika kwa zoezi la uchaguzi mkuu nchini, Ngoma Kizito, ambaye ni mlinzi binafsi wa mgombea ubunge Jimbo la Igunga kwa tiketi ya chama tawala Ndugu Zahoro Panjinga anapotea katika mazingira ya kutatanisha. Baadaye anaokotwa akiwa mahututi na kuwahishwa hospitali. Dokta Malik akiwa anarudi nyumbani baada ya saa za kazi kwisha anapigiwa simu na mtu asiyependa kujitambulisha anampa taarifa za kuokotwa kwa Ngoma Kizito na kumtaka arudi kazini haraka. Dokta anarudi kwa shingo upande.

Isivyo bahati, uhai wa Ngoma unatamatika akiwa mikononi mwake. Lakini kabla hajafariki alimwandikia majina matatu kwenye karatasi bila maelezo zaidi.
Anarudi nyumbani akiwa na ile karatasi pamoja na nakala halisi ya uchunguzi wa kitabibu (*Post Moterm*). Katikati ya uchovu wa majukumu, Mama Ivanna (Mkewe) anazua zogo lisilo na kichwa wala miguu, Dokta Malik anaondoka nyumbani mzima-mzima mpaka kwa *'mchepuko'* wake, Chema Mfaume. Huyu ndiye sababu ya zogo la mara kwa mara baina ya dokta na mkewe.
Usiku wa siku hiyo, vijeba wawili wanavamia nyumbani kwa Dokta Malik, wanamkosa lakini Mama Ivanna ananusurika kubakwa.

Muda mfupi tu, tangu uvamizi utokee nyumbani kwake, Dokta Malik akiwa kwa Chema anapokea simu kutoka kwa yule mtu asiyejitambulisha, akimpa taarifa za uvamizi nyumbani kwake na kumtaka abaki alipo asinyanyue unyayo wala kufanya mawasiliano yoyote. Sasa ni rasmi Dokta Malik anaweka makazi kwa kimada wake. Siku inayofuata, Dokta anakutana kwa siri na yule mtu asiyejitambulisha, ambapo anabadilishiwa mawasiliano. Amri inabaki ileile, kuwa namba hiyo asiwasiliane na mtu mwingine. Ila roho inamfukuta anampigia mkewe kujua usalama wake, KOSA KUBWA!

Baada ya Mama Ivanna kuvamiwa usiku, alidamkia Polisi kutoa taarifa, huko linafunguliwa jalada la uchunguzi, mpelelezi akiwa Kachero Ndalama Mbala. Kwahiyo, alipopigiwa kwa namba mpya na mumewe, papo hapo akampatia namba hiyo Kachero Mbala.

Yeye, alimpa kama mpelelezi, lakini Kachero naye ana yake binafsi tu.

Mpaka hapo, Malengo ya Jeshi la Polisi na ya Kachero Mbala binafsi ni tofauti kabisa!
Suala zima linatua mikononi mwa Kamati ya Ulinzi na Usalama. Vyombo vya usalama vinaingia kazini, huku Jeshi la Polisi na Idara ya usalama kwa upande mwingine.
Yule mtu asiyejitambulisha anamkutanisha Dokta Malik na Kahozya (moja kati ya majina matatu aliyoandika marehemu - Ngoma). Huyu ndio anampa mwanga kiasi juu ya sakata hili.
Dokta Malik alijua amemaliza, kumbe ndio kwanza kumekucha. Bahati mbaya, Chema alimtema, Chaka likaungua. Anajikuta mikononi mwa Kachero Mbala.

Nisikuchoshe, bado hujawajua Kidevu na Nando.
Hujamjua Da' Ruh
Hujamjua Code IO1
Kuna CSE (Computer Science Expert)
Mambo ni mengi.
USIKU WA DENI....Ni deni gani? Nani anatakiwa kulipa?
INAPATIKANA KWA TSHS 10,000/= TU.
PIGA:

**ARUSHA - 0742012182**
**DODOMA - Lugarawa Bookshop 0717996474/0685097713**
**DAR - Kona ya Riwaya: 0655428085**
**NJOMBE -**
**0620152422**



# KITABU: GAMBA LA NYOKA –Ikisiri (7)



**Ikisiri hii imeandikwa na Mwenda Mbatia, nasi tumeiweka hapa kwa msaada wa mtandao ili wanafasihi mjifunze zaidi.**


Jitihada za Mzee Chilongo na wapiganaji wengine wa Kisole ni kazi bure na za kuchekesha kwa sababu serikali inajibu uchokozi wao kwa kuwatumia kikosi cha askari wenye bunduki kuwatia adabu. Mzee Chilongo anazidi kuchekesha kwa jinsi anavyokaidi agizo la askari la kuinua mikono huku wenzake wote wanatii. Anamjibu askari kwa ujeuri: "Mimi siinui mikono juu kubeba mzigo nisiouona!" Anaishia kupigwa buti la kichwani na kuzimia. Askari wanampeleka hospitalini huku wenzake wakipelekwa kwenye boma la Mkuu wa Wilaya ambapo wanaadhibiwa na kufanyiwa dhihaka chungu nzima. Tunaona matumizi ya kinaya cha kiusemi Mkuu wa Wilaya anapowarejelea waliokamatwa kama "Mashujaa wa Tanzania". Hiki ni kinyume cha ukweli kwa sababu wangekuwa mashujaa wasingekuwa bomani wakiadhibiwa. Kwa hivyo hii ni kauli ya kuwacheka kwa ujinga wao wa kujaribu kupigana na serikali.

Ukaidi na uhafidhina wa Mzee Chilongo unazidi kushambuliwa kitashtiti akiwa amelazwa hospitalini. Anayapeleka hospitalini mazoea yake ya kuwatusi na kuwapiga wanawake kwa kumtusi mwuguzi anayesafisha vidonda vya wagonjwa. Kisha anampiga kwa gongo lake na kumuumiza. Mwuguzi anaanguka na kuzimia. Tunaelezwa kwamba Mzee Chilongo anakataa kuomba msamaha "kwa kitendo ambacho alikuwa amezoea kufanya nyumbani" (uk. 45). Ni kitendo kinachofichua alivyojawa na taasubi.

Mzee Chilongo pia anajitokeza kama mwenye mawazo yaliyopitwa na wakati kwa jinsi anavyopinga matumizi ya maji ya bomba baada ya kuzinduliwa kwake katika kijiji cha Kisole. Kufuatia maendeleo haya, kunatolewa agizo la watu wote kukoma kuogea mitoni na visimani na kuanza kuogea uani. Lakini Mzee Chilongo anaona kwamba badiliko hili litashusha hadhi yake kama mwanamume. Anasema:

Nataka kuogea mtoni kwenye maji yatembeayo. Mtoni kwenye samaki na nyoka! Nataka kukoga ziwani kwenye mamba! Mimi sijawa mzee kiasi cha kuletewa maji ya kukoga uani! (uk.123).

Anayatamka maneno haya mbele ya wake zake ili kuonesha udume wake. Masimulizi ndani ya riwaya yanafikia mwisho kwa kuelezea jinsi uhafidhina wa Mzee Chilongo unavyomtumbukiza katika upweke. Kwa sababu amekataa kusonga mbele kimaendeleo pamoja na watu wengine, anabaki nyuma peke yake katika mienendo ya kizamani ambayo haina nafasi katika Tanzania mpya. Hivyo, anapokwenda mtoni kuoga akitarajia kwamba atakutana na wanakijiji wengine, anajikuta peke yake. Hapa ndipo anapochorwa kama kiumbe duni wa kusikitikiwa. Kilele cha matumizi ya ucheshi na bezo kumchora mhusika huyu kinafikiwa anaposhtuka kumuona nyoka mkubwa kwenye miti kando ya mto anamoogelea. Anaokota mawe na kumpiga, lakini Wahusika wa Kitashtiti katika Gamba la Nyoka 125 baadaye anagundua kwamba hakuna nyoka bali gamba lake lililokauka. Mzee Chilongo anajicheka mwenyewe kwa kuingiwa na hofu bure. Gamba la nyoka imetumiwa kama ishara ya jamii ya zamani. Jamii hii ni kama mabaki yaliyotokana na kujibambua kwa jamii ya sasa.




Ujinga wa Mzee Chilongo kubaki katika jamii ya zamani ndio unaoshambuliwa kitashtiti.

**5.0 Hitimisho**

Gamba la Nyoka ni riwaya ya kitashtiti kwa maana ya kwamba imetumia mbinu kadha za utunzi ambazo kwa kawaida huhusishwa na mtindo wa tashtiti. Mbinu hizo ni kama vile ucheshi, bezo, dhihaka na kinaya cha aina mbalimbali. Tumeona pia kuwa kuna mbinu nyingine nyingi ambazo zimetumiwa kufanikisha mtindo wa kitashtiti riwayani. Mbinu hizo ni kama vile; majazi, ishara, sitiari na tashibihi.

Mtindo wa kitashtiti umetumiwa kuwaumba wahusika wakuu ambao ni Mamboleo, Mambosasa, Padri Madevu, Mama Tinda na Mzee Chilongo. Udhaifu wa kitabia wa wahusika hawa na maovu wanayohusishwa nayo umefichuliwa na kusham-

# -SAIKOLOJIA-
# USIWE CHANZO CHA MATATIZO YAKO

**Madame Neema Mbilinyi Mgao,**

**Dodoma,**
**Tanzania.**

**+255 763 013 206.**



Ni kweli kwamba matatizo ni sehemu ya maisha. Sijakataa kuwa matatizo hutukuta binadamu. Ni sahihi kabisa kuwa maisha ya mwanadamu yamegawanyika katika makundi mawili, furaha na matatizo. Ni ukweli usiopingika kuwa matatizo hayaepukiki, hauwezi kuepuka matatizo. Ni sahihi kabisa.

Moja kati ya mambo yanayoleta magonjwa ya afya ya akili au matatizo ya kisaikolojia ni ile hali ya kuandamwa na matatizo kila mara. Hali ya matatizo inapokua mfululu mfululu basi hupelekea mtu kukumbwa na tatizo la afya ya akili au tatizo la kisaikolojia.

Na tuangalie aina za visababishi vya matatizo.

1. **Matatizo yaletwayo kwa kudra au mapenzi ya Mungu.**

Hii ni hali ya kawaida ambayo mtu huwezi kuizuia. Aina hii ya matatizo ndiyo ile unaweza kusema kuwa ni ibada, kama wengi wasemavyo kuwa matatizo ni ibada. Aina hii ya matatizo au mitihani ni ile tunaweza kuita kuwa "haiepukiki". Ni ile hali hauwezi kuiepuka, ni yale mapenzi ya Mungu kwa mja wake anapomtunuku mitihani katika maisha yake.

Mfano wa hayo ni:
a). Maradhi.
b). Kufiwa.
c). Ajali
Na mfanano wa hayo.

Ipo hali ya kawaida kabisa,ambapo inaweza kutokea na ikapelekea matatizo, lakini ipo hali ambayo mtu huona kabisa kuwa hii italeta tatizo lakini bado mtu akadumu katika hiyo hali mpaka akapata matatizo.

2. **Matatizo ya kujitakia.**

Ni kweli kwamba hakuna binadamu anayependa matatizo, lakini, ipo hali ambayo inaweza kumkuta mtu na akaona kabisa kuwa hii inawezekana ikamletea hatari au ikamletea matatizo lakini unakuta mtu huyo bado yumo katika mazingira hayo hayo ya hiyo hatari. Sio kujitakia huko?

Mfano wa hayo ni;
a) Kuvumilia kipigo kwenye mahusiano au ndoa.
Yaani upo kwenye ndoa au mahusiano yaliyojaa kipigo, dharau, kebehi kila siku lakini bado wewe umeng'ang'ana tu. Uking'olewa macho au ukiuliwa sio ulijitakia?.

b) Kuwa na marafiki wapotoshaji.
Kuna marafiki hawana kauli ya kukushauri mazuri, wao ushauri wao ni mbaya muda mwingi, ama hawana uwezo wa kukukataza unapofanya maovu au wakawa wakikushauri kutenda mambo yasiyofaa. Ikiwa mmeshauriana mkachezee kamari hela ya mshahara, ukaliwa hiyo hela, hiyo hali utakayoanza kuipitia utasema ni mpango wa Mungu?

Usiwe chanzo cha matatizo yako kwa kufanya yale mambo ambayo unajua kabisa kuwa ukiyafanya utapata matatizo. Epuka kuwa chanzo cha matatizo yako kwa kuyaepuka madhila yanayoepukika.

Ikiwa unao marafiki ambao unaona kabisa wewe unawamudu, yaani unaona kabisa hao unaoongozana nao hawakohoi kwako, yaani wao kila kitu ni "ndio", nikushauri tu, achana nao hao, watakufanya upate matatizo ya kujitakia.

Tunaishi kwenye dunia iliyojaa mambo mengi mazuri na matamu, lakini pia na mambo mabaya yaletayo matatizo pia yangalipo humo humo. Matatizo yapo pale, nukta moja tu kutoka hapo ulipo au nilipo,ila USIYATAFUTE.

Moja kati ya mambo yanayoleta magonjwa ya afya ya akili ni kuandamwa na matatizo. Matatizo yakimuandama mwanadamu huiathiri akili yake, akili ikishaathiriwa kipi unadhani mtu anaweza kuhimili kuishi vizuri? Hakuna mtu anachoweza kukifanya ikiwa akili yake itavurugwa na matatizo mfululizo .

# -SAIKOLOJIA-
# USIWE CHANZO CHA MATATIZO YAKO

Hakuna kitu unaweza kuzalisha ndani ya akili yako ukishakua kwenye hali ya kuandamwa na matatizo.

**Jinsi ya kuepuka matatizo ya kujitakia.**
1. Epuka makundi yasiyofaa.
Epukana na makundi au marafiki ambao hawakufai, epukana na watu wasio na faida, hilo kundi unaloona unalimudu liepuke haraka. Litakusababishia matatizo ya kujitakia mengi zaidi.

2. Jiwekee mipaka.
Ndiyo, ili kuepuka matatizo ya kujitakia yafaa kujiwekea kiasi au mipaka katika kila jambo ulifanyalo. Ukiwa na mipaka katika mfumo mzima wa maisha yako ni dhahiri shahiri utaepukana na mambo mengi sana. Mfano, wewe ni mnywaji, na ukishakunywa inakupelekea kupiga wengine hadi asubuhi unajikuta anaamkia kituo cha polisi, ukijiwekea mipaka au kikomo au ukiwa na kiasi ni wazi kuwa japo utakunywa ila utajiwekea mipaka kuwa uishie chupa au kiwango fulani.

3. Jisikilize.
Kuna ile hali ya kuisikia sauti ndani yako, ile hali unataka kufanya hivi ghafla roho ikakataa, basi ili kuepukana na matatizo ya kujitakia basi jipe nafasi ya kujisikiliza.

4. Shaurika.
Kuna namna baadhi ya watu wamebahatika kupata watu wa kuwashauri. Chukulia mwanamke au mwanaume aliyeoa au kuolewa, akashauriwa asiwe na mahusiano nje ya mke au mumewe, au ushauri mwingine wowote uujuao. Ikiwa unapata watu wakakushauri basi shaurika. Pokea ushauri wao, uchekeche kama unakufaa. Baada ya kuuona kuwa unakufaa basi ufuate. Shaurika, hakuna anayejua kila kitu.

Nikutakie mwaka mpya mwema,Mungu atuangazie nuru yake, atuepushe na matatizo ya kujitakia na hata yale anayotupitisha kwa maana ya tuwe karibu nae (matatizo ni ibada, usikufuru unapoyapitia, mwombe Mungu, mshukuru, msifu) Mungu atupunguzie makali yake .

Mwaka 2024 ukawe mwaka mzuri, wenye mafanikio,na wenye baraka tele. Mungu atubariki sote.

**Happy new year.**

Kwa mazungumzo na ushauri wa kisaikolojia, tuzungumze kupitia:-

Simu namba +255 763 013 206.
Au WhatsApp no. +255 746 139 654.

Karibu sana , tuzungumze tu, zungumza na mimi, kwa pamoja tuyafanye maisha na dunia iwe mahali salama kwa kuishi.
Karibu.



# HADITHI: NILIMUUA DADA NIOLEWE NA SHEMEJI-13



**Siku hiyo ilikuwa kama imepigwa laana na kukosa baraka za Mwenyezi Mungu. Watu walikuwa wachache ingawa taarifa zilipelekwa kwa watu wengi. Kwa ujumla haikufana kama ile siku ya ndoa ya dada.**

Nilijiona mjinga na mtu asiyejua atendalo. Niliangalia zaidi leo nikashindwa kufikiria kesho. Nilifanya uamuzi wa asubuhi nikasahau kuna mchana, jioni na usiku. Sikuona sababu ya kumuua dada kama mambo yenyewe ningalijua yangalikuwa hivi. Hakuna zawadi, hakuna karamu wala tafrija. Ndugu hawakuwepo. Bila shaka ilikuwa laana ya dada.

Ndoa ilipita salama usalimini licha ya kuwa kama nimesusiwa na watu wangu wa karibu. Nilianza rasmi maisha ya ndoa nikiwa na mume wangu aliyekuwa shemeji yangu.
Siku ya kwanza kuingia ndani nikiwa kama mke halali wa shemeji nilikutana na balaa ambalo lilinifanya nitake kurudi nyumbani kwa mama na baba. Nilivyoteremka tu kwenye gari nikiambatana na mume wangu na baadhi ya watu hadi ndani. Nilipofika sebuleni nilikutana na vimbwanga. Nilimkuta dada amekaa kwenye sofa akiwa ameji-inamia. Aliponiona akasimama huku akiwa na hasira ambazo sijawahi kumuona nazo wakati wa uhai wake. Alinijia kwa kasi huku akininyooshea kidole na kutamka maneno ambayo sikuyasikia. Nilipiga kelele kubwa lakini hakuna aliyenisikia zaidi yangu mwenyewe. Watu walionisindikiza waliendelea na vigelegele na shangwe zao.

Mbio za dada ziliishia miguuni mwa mume wangu. Alipiga magoti huku akinyoosha mikono juu kama mtu aombaye msamaha huku akilia. Masikini, hakuna aliyemsikia wala aliyemuona zaidi yangu. Alilia sana hadi nikaingiwa na huruma nami nikaanza kulia kumsaidia dada yangu kipenzi. Kadiri nilivyolia ndivyo shangwe na vigelegele vilivyoongezeka. Nikatamani niende alipo nikamuinue ila nilishindwa.

Baada ya watu kuondoka ndani tulibakia watu wachache; mimi, mume wangu na mtoto wa shangazi yake pamoja na dada yangu wa mama mdogo. Ulipoingia usiku balaa likawa zaidi ya mchana. Usiku huo kabla ya kulala, tuliingia bafuni kule kule chumbani kwetu. Baada ya kuoga mume wangu alikuwa wa kwanza kutoka halafu nikafuata mimi. Nilipofika chumbani niliyakuta maajabu mengine ambayo hasa yalinifanya nitamani kurudi nyumbani usiku huo wa siku ya kwanza ya ndoa yangu.

Nilimkuta mume wangu amelala kitandani akinisubiri kwa hamu kubwa. Nilipoangalia vizuri kitandani nilimuona dada akiwa amelala ubavuni kwa mume wangu. Nilibaki nimeshangaa nisijue la kufanya. Nilikodoa macho kwa wasiwasi na woga.

“Vipi mbona umesimama hivyo? Njoo tulale.” Aliniambia mume wangu baada ya kuniona nimesimama nikipigwa butwaa. Nilitamani kumwambia nilichokiona ila sikuthubutu. Hata kusogea kitandani sikuthubutu.

Mume wangu aliendelea kunishangaa. Alinifuata nilipo akanishika mkono halafu alinivuta taratibu kuelekea kitandani. Awali nilikuwa mbishi. Baadaye nilikubali baada ya dada kutoweka kitandani na hakuonekana. Nilipanda kitandani, naye mume wangu alipanda. Bado hofu kubwa ya kutokewa na dada ilinitawala. Dada hakutokea wakati huo hadi majira ya saa saba usiku. Alinitokea nikiwa usingizini. Nilimsikia akilia huku akilalamika.

“Yaani mdogo wangu unathubutu kulala na shemeji yako wakati nashuhudia? Jamani nimekukosea nini hata malipo yake yakawa hivi?” Nilishtuka toka usingizini nikaangaza chumbani. Nilimuona dada amekaa kwenye mfumbati wa kitanda akilia sana kwa uchungu. Aliponiona nimeamka aliniangalia kwa huzuni halafu akaniambia, “Unafahamu kabisa huyo ni shemeji yako na tuko katika ndoa. Umeona raha kulala naye nikishuhudia.”

Aliinuka alipokuwa amekaa akanijia. Aliponikaribia akainua mkono kama anataka kunipiga kibao. Nilipiga kelele.

“Aaaa nakufaaaaaaa!” Mume wangu alishtuka. dada alitoweka baada ya kelele zile.

"Vipi, kuna nini?" Aliniuliza.
"Nimeota ndoto mbaya sana." Nilimdanganya.
"Pole sana. Ni ndoto tu isikusumbue. Tulale mke wangu usiku mwingi huu." Akaniambia mume wangu kwa upendo.

Baada ya tukio la usiku huo dada hakutokea mara kwa mara. Nilirudi tena kwa mganga kule Bagamoyo ambako alinifanyia tambiko ambalo aliniambia amemfunga, hatoweza kunitokea tena na kunikosesha amani. Mganga aliniambia kwamba, ili asiendelee kunitokea, natakiwa nipeleke shilingi kumi ya sarafu kila ifikapo tarehe ishirini na tano ya kila mwezi kwa muda wa miaka mitatu mfululizo. Baada ya hapo maisha yangu yatakuwa salama na yenye furaha.

Nilitamani sana kuishi maisha ya raha na amani. Nilivyoambiwa hivyo sikuwa na shida ya kutotimiza. Haraka nilikubaliana na mganga kisha nilirejea nyumbani kuanza kuyafurahia maisha ya ndoa kwa kuwa nilitamani sana kuolewa na huyu niliye naye.
Wakati huo alikwishahitimu Shahada yake ya awali ya Sayansi ya Jamii. Pia alipandishwa cheo kazini kwao na kuwa Afisa Uhusiano wa Umma. Kwa nafasi hiyo hakuwa anatembea mara kwa mara kwenda kwenye tafiti bali alisafiri nje ya nchi hasa shirika lao linapotakiwa kupeleka takwimu ya shughuli zao Umoja wa Mataifa na kuomba ufadhili.

⚜

Masharti ya mganga yalikuwa mepesi kuyakubali, lakini magumu kuyatekeleza. Kupeleka shilingi kumi kila tarehe ishirini na tano ya kila mwezi kwa muda wa miaka mitatu haikuwa kazi rahisi. Niliweza kutekeleza kwa mwaka wa kwanza tu tena mwaka huo nilitekeleza kwa kusuasua. Nilijitahidi sana kutimiza nilichoambiwa na mganga ili niishi kwa amani na furaha, lakini sikuweza.

Mwaka huo wa kwanza niliumaliza kwa matatizo. Mganga alinionya kuwa dada hakufa. Alikuwa sehemu tu amefanywa msukule. Hivyo, kutotimiza masharti kwa wakati kutasababisha lile tambiko kutofanya kazi kikamilifu. Endapo tambiko halitofanya kazi kikamilifu dada atanitokea tena na hiyo haitakuwa na kinga tena. Itakuwa ni kuumbuka. Ataonekana na watu wengi. Kwa hiyo nilijitahidi sana. Niliumaliza mwaka wa kwanza kwa namna hiyo. Sasa nilikabiliwa na miaka miwili mbele yangu. Hapo ndipo paliingia mtihani – mtihani ambao sitakuja kuusahau katika maisha mpaka nitakapoingia kaburini.

Ndoa yetu ilikaribia miaka miwili. Katika kutimiza miaka hiyo miwili ni mwaka mmoja na miezi sita ndiyo nimefanikiwa kupeleka shilingi kumi kumi kwa mganga. Baada ya hapo nilitakiwa kusafiri na mume wangu kwenda Marekani. Mume wangu alitakiwa kuwa huko kwa miezi miwili mfululizo. Hivyo, aliomba kazini kwake kuambatana nami. Nilipoletewa taarifa hiyo nilifurahi kwa upande mmoja na upande mwingine nilishtuka sana. Nilifurahi kwa sababu sikuwahi hata siku moja kuwaza kufika Marekani. Hiyo ilikuwa nafasi pekee kufika huko. Pia nilishtuka kutokana na kuwa nitakuwa nchini humo kwa miezi miwili mfululizo. Hivyo, sitopeleka shilingi kumi kwa mganga katika miezi hiyo miwili. Jambo hilo lilinifanya nifikirie sana kukataa kwenda Marekani na mume wangu. Japo nilikuwa na sababu ya kutokwenda sikuweza kuiweka hadharani.
Ilikuwa sababu ya moyoni mwangu. Ni mimi pekee nilitakiwa kuijua. Nje ya moyo wangu sikuwa na sababu ya kujitosheleza kukataa.

Hivyo, nilikwenda kwa mganga kumueleza jambo hilo. Hapo ndiyo nilichoka kabisa. Mganga aliniambia kuwa alijitahidi kufanya dawa zake mizimu ikamwambia ikitimia miaka miwili tu inatosha. Nitakuwa nimeshinda vita. Hii ilimaanisha hakutokuwa na haja ya kumalizia mwaka wa tatu. Alisema mizimu ilimwambia pia kuwa, ili dawa zikubalike nilitakiwa kupeleka hizo shilingi kumi kumi bila kukosa ama kuchelewesha kila mwezi. Kuondoka kwangu kwenda Marekani itakuwa balaa kubwa.

ITAENDELEA





**Muammar Abu Minyar Al Gaddafi**

## Elimu na harakati za kisiasa: 1950-1963

Elimu ya awali kabisa ya Gaddafi ilikuwa ya kidini, iliyotolewa na mwalimu wa Kiislam wa eneo hilo. Baadaye, alihamia Sirte, karibu, ili kuingia shule ya msingi, alisoma madarasa sita katika miaka minne. Elimu nchini Libya haikuwa bure, lakini baba yake alifikiri ingemnufaisha sana mwanawe licha ya matatizo ya kifedha. Katikati ya wiki Gaddafi alilala msikitini, na mwishoni mwa wiki na likizo ilimpasa kutembea maili 20 (kilomita 32) kuwatembelea wazazi wake. Ingawa babake Gaddafi hakusoma, lakini alijitolea sana kumpeleka mtoto wake shule. Akiwa **B**edui maskini, Gaddafi alikabiliana na unyanyasaji na ubaguzi kutoka kwa wanafunzi wenzake waliokuwa wakiishi jijini.

Gaddafi, alikuwa na walimu wengi wa Kimisri ambao walimjulisha kuhusu matukio makubwa yaliyotokea katika nchi yao. Kutoka Sirte, yeye na familia yake walihamia katika soko la mji wa Sabha huko Fezzan, Kusini-Kati mwa Libya, ambapo baba yake alifanya kazi kama mlezi wa kiongozi wa kabila wakati Muammar akihudhuria shule ya sekondari, jambo ambalo wazazi wake hawakufanya. Gaddafi alikuwa maarufu katika shule hii; baadhi ya marafiki zake aliokuwa nao huko walipata kazi muhimu katika utawala wake wa baadaye, hasa rafiki yake mkubwa, Abdul Salam Jalloud.

Walimu wengi huko Sabha walikuwa Wamisri, na kwa mara ya kwanza, Gaddafi alipata kusoma magazeti ya Kiarabu kutoka kwao kusikiliza na matangazo ya redio, haswa Sauti ya Waarabu ya Cairo. Alipokuwa akikua, Gaddafi alishuhudia matukio muhimu yaliyotikisa ulimwengu wa Kiarabu, ikiwa ni pamoja na Vita vya Waarabu na Israeli vya 1948, Mapinduzi ya Misri ya 1952, Mgogoro wa Suez wa 1956, na kuwepo kwa muda mfupi kwa Jamhuri ya Umoja wa Kiarabu (UAR) kati ya 1958 na 1961. Gaddafi alifurahia mabadiliko ya kisiasa yaliyotekelezwa katika Jamhuri ya Kiarabu ya Misri chini ya shujaa wake, Rais Gamal Abdel Nasser. Nasser alitetea utaifa wa Waarabu; kukataliwa kwa ukoloni wa Magharibi, ukoloni mamboleo, na Uzayuni; na mabadiliko kutoka ubepari hadi ujamaa. Gaddafi aliathiriwa na kitabu cha Nasser, *Philosophy of the Revolution,* ambacho kilieleza jinsi ya kuanzisha mapinduzi. Mmoja wa walimu wa Misri wa Gaddafi, Mahmoud Efay, aliripotiwa kuunga mkono mawazo ya vijana ya kisiasa, na akamshauri kwamba mapinduzi yenye mafanikio yangehitaji kuungwa mkono na jeshi.

Gaddafi alipanga maandamano na kusambaza mabango ya kukosoa utawala wa kifalme. Mnamo Oktoba 1961, aliongoza maandamano kupinga kujitenga kwa Syria kutoka UAR na kuchangisha pesa za kutuma msaada kwa Nasser. Wanafunzi 20 walikamatwa kutokana na machafuko hayo. Gaddafi na wenzake pia walivunja madirisha katika hoteli moja ya eneo hilo ambayo ilishutumiwa kuuza pombe. Ili kumwadhibu Gaddafi, mamlaka ilimfukuza yeye na familia yake kutoka Sabha.

Gaddafi alihamia Misrata, huko akisoma Shule ya Sekondari ya Misrata. Akidumisha shauku yake katika uharakati wa utaifa wa Waarabu, alikataa kujiunga na chama chochote cha siasa kilichopigwa marufuku mjini humo—pamoja na vuguvugu la *Arab Nationalist Movement, Arab Socialist Ba'ath Party,* na *Muslim Brotherhood*—akidai kwamba alikataa ubinafsi wa makundi. ***Itaendelea..***

# SAKO KWA BAKO:

## Eva Mrema: Kungwi mpaka kwenye vitabu

*EVA MREMA au nikuite Kungwi... aisee Kungwi ni jina zito sana. Yaani nikirudisha mawazo nyuma nikifikiria wale makungwi wa enzi zile tunaowajua kama makungwi walivyokuwa wazee, watu wazima, sura zao hazina ushirikiano... enh... Sasa we kungwi kivipi yani, jieleze kwanza...*

Jina langu ni Eva Mrema, marafiki zangu huniita Malkia wa tabasamu. Wadogo zangu wa kike huniita Kungwi wa kisasa. Nadhani hapa kwenye 'u-kisasa' ndo kunabadili ile dhana yote ya ukungwi wa kizamani.



*Ok! Hebu nambie, kwanini Kungwi?*

Halikuja bahati mbaya jina hili. Limeanzia kwenye kitabu nilichokipa jina hilo KUNGWI. Na limekomazwa na kupata umaarufu baada ya kuthibitisha ukungwi kwa wanawake waliofanikiwa kupata darasa kwangu.

*Sawa, nafikiri unaanza kueleweka taratibu. Kumbe kitabu cha KUNGWI kikakupa u-kungwi. Enhe...u-kungwi na uzuri wa sura vina uhusiano?*

Havina uhusiano. Ukungwi ni tafsiri tu na dhana iliyojengwa kitambo ya kuhusishwa na mambo kadha wa kadha ila uhalisia ni kwamba, KUNGWI ni mkufunzi wa mabinti na wanawake juu ya wajibu, majukumu na yote wanayotakiwa kuyajua kuhusu maisha, ndoa na jamii. Mwanamke mwenye maarifa na uzoefu wa mambo hayo ukiweka kando kigezo cha umri anaweza kuwa Kungwi. Kwa muktadha huu sura na ukungwi havina uhusiano.

*Nimesikia juu juu tu kuwa umeandika kitabu, na mimi ninaamini kuwa yeyote anayeandika kitabu basi ni msomaji mzuri wa vitabu. Nambie ni vitabu gani wapendelea kusoma?*

Nimeandika vitabu, siyo kitabu. Hadi sasa nina riwaya sita na vitabu vya maarifa kwa mwanamke viwili. Mimi ni msomaji mzuri wa vitabu. Nasoma vitabu vya aina tofauti. Sijayakita mapenzi yangu ya kusoma kwenye aina fulani maana maarifa hayana upande mmoja. Napenda kujua mambo mengi, hivyo nasoma vitabu na riwaya aina zote.

*Kitabu chako kinaitwaje? Na nini kilikusukuma kuandika kitabu hicho?*

Vitabu vilivyo gumzo duniani kutoka kwangu sasa ni viwili. MWANAMKE WA THAMANI NDANI YANGU na KUNGWI. Kama nilivyotangulia kusema ni vitabu vya elimu na maarifa kwa mwanamke. Nimeanza na upande niupendao. Tuko kwenye dunia ambayo ina elimu ya darasani zaidi ya ile ya maisha na wakati huku mtaani tunaishi zaidi ya kusoma. Sambamba na elimu ya shuleni. Mwanamke anahitaji elimu hai ya maisha.

*Je kuandika kitabu hicho kulitokana na kazi yako ya u-kungwi au vitabu ulivyosoma?*

Kitabu cha MWANAMKE WA THAMANI NDANI YANGU ni maono ambayo nimekuzwa kwayo kwa kitambo. Humo kuna majibu ya maswali ya binti yeyote ambaye atakuwa mwanamke. Huko kuna muongozo wa kujitambua binafsi kwa mwanamke yeyote ambaye hakupata maarifa ya kujijua vyema na kujipenda vya kutosha na kauli yangu juu ya mada zilizo ndani ya kitabu: 'HAKUNA MTU AMBAYE ANAWEZA KUTOA KILE AMBACHO HANA KWA HAKIKA" utatoa upendo siku ukiweza kujipenda vizuri.

Kitabu cha KUNGWI ni muendelezo wa maono. Ukimponya mtu nafsi na usipompa maarifa ya kumsaidia kuendelea au kumudu kuishi kwa kuwajibika utakuwa haujamsaidia bado. Kwenye Kungwi ni swala la kuwajibika kuanzia kwa mwanamke binafsi hadi kwenye ndoa, na ndani zaidi ya ndoa.

*Asante sana Eva Mrema, 'Kungwi Mrembo' tuna mengi ya kuongea… naamini panapo uhai nitakujia tena bado nina mambo ambayo nataka msomaji ayajue toka kwako.*

# KISASI CHA HISIA— 03

**Hapo enjo alitembea hadi kwenye kabati na kuchukua ile bahasha na kumkabithi Steve. Steve aliipokea na kuifungua kisha akaanza kuisoma jinsi ilivyoandikwa...**

*Dear Steve*
*Kwa muda mchache niliokuwa na wewe nimenifunza ya kuwa watu wachache wenye moyo wa huruma bado mnaishi, Asante kwa kujitoa kwako kunitafuta mimi mpumbavu wa hisia.*
*Najua hali yangu ambayo nilikuwa nayo toka siku ile nimeenda hospitali na kunieleza hali halisi ya mwenendo wa mwili wangu, siku nakuona nililia kwa mawili Moja ni kuchelewa kuonana na weewe mpaka mwishoni mwa uhai wangu na mbili umekuja kama suprise na mimi ninaondoka kama suprise.*
*Katika maisha yangu nimekutana na watu wema na wabaya kwa wakati mmoja wewe umekuwa rafiki yangu wa mwisho mwema kukuona.*
*Kama utakuwa na mpango wa kufanya kisasi chochote katikati ya haya yote yaliyotokea nimekuandikia barua hii kukusihi usisahau kuzilipia hisia zangu kisasi chake.*
*Nilitamani kuendelea kukuona ukiwa kama mfariji wangu lakini kifo nacho kilikuwa karibu yangu muda wote Baraka zangu na kivuli changu kipo kwako nenda kawaonyeshe SUPRISE YA MAUMIVU.*

Huo ndio ulikuwa waraka uliomtoa machozi Steve huku akiwa katikati ya hisia mbaya na nzuri, aliwaza ni *suprise* gani inayoweza kubeba maana kamili ya maumivu aliyoyapitia? Hakuona Ni wakati huo Enjo alikuwa yupo pembeni ya Steve lakini hakuweza kusema chochote huku akishuhudia machozi kama mfereji yakitoka kwenye macho ya Steve.

"Enjo" Steve aliita
"Abeee"
"Unaweza ukanisaidia jambo moja tu"
"Jambo gani"aliuliza Enjo
"Nataka niwaoneshe ladha ya maumivu aliyoyapitia Dayana, pia na mimi niwaoneshe ile shubiri niliyoinywa mchana wa jua kali, kile kicheko cha Rachel wakati mimi nalia imefika mwisho nataka yeye aliye na mimi nicheke. Kisasi kina



njia zake acha kijitafute chenyewe lakini mkononi mwangu nina *suprise* zao zote walizonipa. Nina kifurushi cha *suprise* lazima niwafikishie" Steve aliongea huku anatetemeka

⚜

Ilikuwa imepita wiki tangu Dayana apoteze maisha. Sasa ulikuwa umebaki urafiki wa Enjo na Steve huku mikakati ya kisasi ikiendelea
"Eeeh kasemaje kwani"aliuliza Steve
"Kasema tukutane saa kumi Live bar & Guest House" alijibu enjo
"*Ok* tangulia wewe weka mipango sawa kisha utaniambia kama kila kitu kipo tayari" Steve akasema.
"Sawa hakuna shaka toka jana nilikuwa nimelipia chumba hivyo kila kitu kipo tayari"
"Sawa kazi njema"aliongea Steve

⚜

Wakati wakiendelea kuwaza ni namna gani watafanya kisasi chao ndipo Enjo alikuja na njia iliyoungwa mkono kama njia sahihi ya kufanya malipo
"Unajua kipindi Lucas alikuwa anatoka na Dayana pia alikuwa ananitaka na mimi" alianzisha maongezi.
"Kweli? Kwahiyo ilikuwaje"aliongea steve
"Nilimkatalia lakini huu naona unaweza ukawa mwanya wa kulipa kisasi"
"Unataka tufanyeje sasa hapo, njia yako ni ipi unayoiona inafaa kwa sasa?" Steve akauliza.
"Kwa sasa nitamtafuta nitamwambia hata mimi nilikuwa nampenda ila kwa kuwa Dayana alikuwepo nilishindwa kumkubali, lakini sa'ivi Dayana hayupo basi nipo tayari" wazo likawekwa mezani
"Eeh baada ya hapo akikubali itakuwaje"
"Tutaweka *camera* kwenye kile chumba chetu ambacho nitamuelekeza aje na akija tu sitafanya nae chochote ila nitamchezea huku tunarekodiwa kisha nikimaliza yangu zile video nitakuelekeza cha kufanya"aliongea Enjo
"Aah sawa hapo nimeelewa, kazi ianze" Steve akaunga mkono.

Baada ya mpango wao kukamilika sasa ilikuwa inasubiriwa saa kumi tu ili waweze kutekeleza azma yao

# KISASI CHA HISIA — 03



iliyokusudiwa kufanyika
Kweli Mungu si Athumani baada ya saa kumi Lucas aliingia mtegoni kichwa kichwa kisha akapewa juisi iliyochanganywa na madawa ya kulevya baada ya kunywa alikuwa kama amelewa lakini bado yu mzima kama mtu aliyelewa tu.
Baada ya hapo Enjo alifanya kile kitu amekusudia kisha aliondoka na kumuacha Lukas akiwa uchi kama alivyozaliwa.
Enjo alimtumia Rachel *sms* iliyosomeka *"Nenda live bar kamchukue mumeo chumba no 12"*
Hiyo ilikuwa ni namba ngeni iliyosajiliwa maalum kwa ajili ya kuimaliza kazi yao iliyokuwa sasa ipo ukingoni, suala la kwanza likawa limekamilika sasa likafuata suala la pili.

Ilikuwa ni siri sana ambayo Dayana aliamua kuifanya siri yake peke yake lakini baadae baada ya Enjo kumsimulia ya kuwa Lukas anamtaka alimuweka wazi ya kwamba yeye ni muathirika wa Ukimwi ambao aliupata kwa huyo huyo lukas na sasa Lukas anafanya kuusambaza tu kwa wengi. Suala la pili lilikuwa ni kumwambia Rachel ya kuwa sasa ajiandae kutumia doze hapo pia sms ikatumwa,

*Ukitoma live bar nenda hospital ukachukie Doze ya Ukimwi kwa ajili ya kuanza kutumia.*
Ni hii sms iliyomfanya Rachel azimie masaa kadhaa kabla ya kuzinduka na kuzima tena na sasa alikuwa yupo kwenye majuto makuu.
Ya Tatu ilikuwa ni kutafuta namba za wazazi wa Rachel kisha na wazazi wa Lukas, wachungaji na wazee wa kanisa Pamoja na ndugu wa karibu wanaotumia mtandao wa *whatsApp* kisha wote wakawekwa kwenye group moja na kutumiwa video za Lukas huku zikiambatanishwa na maneno yaliyosomeka
*NA HII NI SUPRISE YA MAUMIVU*
ilikuwa ni aibu kubwa sana kuwahi kutokea. Rachel aliishia kuwa nusu mzima na nusu chizi kwani alikuwa haamini kama tayari ameshaupata Ukimwi.
Lukas alihama mji na hakukulikana ni wapi aliendaa
Steve alioa mwaka mmoja mbele huku Enjo yeye aliolewa miezi sita baada ya kumaliza kisasi cha rafiki yake.

**MWISHO**



# RIWAYA: CRONOC 7 (10) - richard MWAMBE

*Ilipoishia...*

**Chumba kilikuwa na mwanga mzito mwekundu na wote walikuwa ndani humo walivalia mavazi mekundu na kufanya kwa namna moja au nyingine kutoelewana vyema sura zao, na hii ilizidishwa na kuta za chumba hicho, maana nazo zilikuwa na vioo vilivyozidisha rangi hiyo.**

***Endelea…***

Aliyekuwa kama kiongozi kati yao aliinua uso wake na kutazama jopo lililofika la wajumbe saba.

"Nani anayetuua?" akauliza, "Afrika lazima mtueleze mazingira ya vifo hivi vya ghafla, na inawezekanaje mtu kupenya kwenye ngome zetu kirahisi namna hiyo?" akaongeza swali.

Ukimya ukachukua nafasi.

"Mnajua tuna mipango mikubwa sana ya kuchuma pesa nyingi katika serikali mbalimbali za dunia kwa njia zetu zile za kila siku… Serikali na viongozi wenu tunao na tumeomba uangalizi wa hali ya juu katika usalama wa watu wetu, kwa nini haya yanatokea huko Kenya?" akazidi kuongea.

"Kiukweli mpaka sasa hatujui…"

"Siyo hatujui, sema hujui!" akamkatisha kauli yake.

"Patrick Njuwe ameuawa kwa risasi, na Zuganji kwa sumu, lakini kutoka katika mauaji ya Zuganji tunaweza kumpata muuaji kwani mtu wa mwisho kuonana naye hata picha yake imepatikana," mjumbe mwingine akaeleza ambaye alikuwa Nairobi kwenye kikao cha siri ambacho mara baada ya kuisha ndipo mauaji hayo yalipotokea.

"Naanza kuwa na wasiwasi, na nahitaji mtu mmoja auawe haraka iwezekanavyo. Mjumbe aliyejitenga kutoka Cronoc 7 anaweza kuwa ni chanzo cha vifo hivi," akalieleza jopo. Na hapo minong'ono ikaanza kati ya wajumbe wakionekana kama wamefunuliwa jambo fulani hivi ambalo hawakulitegemea.


"Niliwahi kufikiri hilo, lakini sikuweza kulisema wazi kwani kwa kiapo chetu huyu mtu alishajitoa na tumenyang'anya kila haki yake. Swali ni kwamba kwa nini awe adui yetu?" akauliza mjumbe.

"Jibu rahisi, anaujua mpango wa Millenia, je kama kaamua kujitoa ili atushambulie kwa nje na kisha aharibu kabisa mipango yetu. Kumbuka na yule mjumbe aliyejitoa mwaka ule… na yule mwingine, sasa wako wanne nje ya kundi. Natoa oda wauawe wote wanne kabla hatujapata madhara zaidi kwa maana najua hawa ndiyo wanaotushambulia. Haiwezekani mtu asiyetujua kutushambulia sisi. Lazima muuaji au mwenye kauli ya uuaji anatokea humu au aliwahi kuwa humu. Hata nilipoongea na Mkuu amesadiki hilo," alipomaliza kusema hakuchukua muda akasimama wima na wale wengine nao wakasimama.

Kisha taa zikazimika na zilipowaka hakuwepo kati yao, mjumbe mmoja baada ya mwingine walianza kutoka katika ukumbi ule na kuelekea mjini tayari kwa kazi inayowakabili maana kwa kusema hayo na kutoa maagizo ya namna hiyo tayari mhusika alishajua nini anatakiwa kufanya.

Saa tatu baadae

Baridi kali ilikuwa ikiendelea kuliadhibu jiji la London, kila aliyeonekana ama alikuwa na jaketi zito au sweta kubwa la manyoya ya kondoo ili kupambana na hali hiyo. Daima katika nchi za ukanda huo




mwezi wa December mpaka March au hata April tabu kubwa kwao huwa ni baridi.

Katikati ya daraja kubwa la kihistoria; lenye kujulikana kila kona ya dunia, lenye uwezo wa kufunguka endapo meli kubwa itataka kupita hapo, mwanaume mmoja, mzee wa makamo alikuwa akipita kutoka upande mmoja kuja mwingine. Mikono yake ikiwa ndani ya koti lake na sigara ikichomoza vyema kinywani ikibanwa sawia kwa papi za midomo yake.

Alipofika katikati kabisa ya daraja hilo alipigana kikumbo na mtu mwingine aliyekuwa akienda upande ule aliokuwa akitoka yeye na katikati yao ikaanguka bahasha moja nyeupe. Bila kujali yule mtu akapita na yule mzee wa makamo akasimama kwa sekunde kadhaa akiangalia ile bahasha pale chini. Akatikisa kichwa na kuiokota kabla haijadakwa na unyevunyevu kisha akamtazama huyo aliyeiangusha akipotelea mbali. Alipoona watu wote wapo kwenye shughuli zao, hakuogopa kuifungua na kuchungulia ndani. Hakukuwa na

kitu zaidi ya picha nne za watu tofauti. Akaelewa kuwa wito alioupokea dakika chache zilizopita hakutakiwa kuutimiza na kwa maana hiyo umeishia hapo, akamtazama tena yule mtu aliyepigana naye kikumbo, asimwone.

⚜

Mr. Codec Smith, mtu mzima wa miaka sitini, mwanajeshi mstahafu katika jeshi la Uingereza, ambaye kwa miaka mingi amehudumu katika jeshi la kujihami la nchi za Ulaya, NATO, aliondokea kuwa muuaji mashuhuri wa kukodi. Mauaji mengi aliyowahi kuyatekeleza hayakuwahi kushukiwa hata siku moja kwa jinsi alivyoijua kazi hiyo na kuifanya kwa weledi wa hali ya juu.

Asubuhi ya siku hiyo alipokea simu ambayo yeye aliita ‘simu ya siri’, ikimtaka kufika Mc Donald Café, London, ndani ya nusu saa tu. Lakini, mpaka hapo alielewa kilichokuwa kikiendelea. Akazidi kuvuta hatua za taratibu na kulimaliza lile daraja. Mbele kidogo aliiacha barabara hiyo na kupita katika mtaa mdogo mpaka upande wa pili kulikokuwa na jengo kubwa la kibiashara na kuingia ndani yake.

Alipitiliza moja kwa moja mpaka maliwato na kujifungia humo, akachomoa simu yake ya mkononi na kuchukua moja ya picha ambayo nyuma yake ilikuwa na namba fulani, akabofya ile namba na kuiweka sikioni.
“…Didiof Martis… Nigeria, Anambra State plot namba 650… Eliminate him…”
Ujumbe ulisikika katika simu ile mara tu baada ya kubofya ile namba. Hawa jamaa wamejipanga mpaka kwenye sekta ya mawasiliano. Akawaza huku akiirudisha ile picha kwenye ile bahasha na kuifutika kwenye koti lake kubwa, akatoka na kupotelea mjini. Codec hakutaka kuangalia hao wengine, kazi yake alipenda kuifanya hatua moja baada ya nyingine. Kichwani mwake alishajipanga kuwa akimaliza kazi ya Nigeria ndipo atachukua picha nyingine kujua nini la kufanya. Mara zote alizoea kupewa kazi ya kuua mtu asiyezidi mmoja lakini wakiwa wengi zaidi basi ni wawili, lakini ilimshangaza mara hii kupewa watu wanne kwa mara moja. Nje ya Jiji la London katika barabara kuu inayoelekea Manchester, Codec alikuwa ametulia katika nyumba yake ndogo ndani ya chumba kidogo ambacho mlango wake ulikuwa na maandishi ‘Hell’.

Ndani ya chumba hicho alikuwa amebandika picha za watu mbalimbali ambao alikwishawatoa uhai kwa mkono wake mwenyewe. Kila alipoziangalia picha hizi nafsi yake ilitulia. Codec alipenda kuua kuliko kitu kingine chochote kile katika maisha yake. Akautazama mkono wake kisha akatikisa kichwa na kuinua begi lake, akaondoka na kuufunga mlango nyumba yake.

⚜

Amata na Madam S walikutana Shamba kwa siri. Kikao kifupi kilichokuwa na maamuzi mazito ndicho kiliwakutanisha.
“Na hapa ndipo ninapochanganyikiwa…” Madam S akamwambia Amata.
“Kwa nini au nikuulize kwa vipi?”
“Askofu Bariki hajafika London, yaani hajaonekana kabisa pale uwanja wa ndege,” akaeleza huku akiliweka kando kabrasha alilokuwa akilichungulia. Muda wote ambao Madam S alikuwa akieleza hayo Amata zaidi ya kuuliza au kujibu basi hakuongea lolote.
“Amata, tunafanyaje juu ya hili?” akamtupia swali. Badala ya kujibu akachukua karanga kidogo kutoka kwenye kibakuli cha udongo kilichokuwa hapo mezani na kuzirushia kinywani moja moja kisha akaketi sawasawa huku bastola zake zikionekana waziwazi kutulia kwenye mikanda maalum aliyoivaa mwilini juu ya fulana yake.

“Mi nasubiri tu mniambie cha kufanya, kama tafutishi mnazo za kutosha. Iliyobaki hapo ni kuanza matembezi kuona ukweli wa hivi vilivyopo na kupata mengine mengi kisha tutajua tunafanyaje,” akamwambia.
“Ok, nimekuelewa kijana wangu, sasa kila mmoja ana jukumu lake juu ya hii kitu, na wewe nataka nikupe jukumu lako…”
“Sawa!”

*ITAENDELEA...*

**Kitabu cha CRONOC 7—chapa ya pili kitakuwa madukani muda wowote kutoka sasa.**

**Weka oda yako sasa kwa kutuandikia whatsapp 0766974865.**

**Na ukipenda kulipia kabisa waweza fanya hivyo kwa kutuma pesa ‘12,000/=‘ kwenda Mpesa Lipa Namba 5559006 JAMVI LA SIMULIZI kisha tutumie meseji ya muamala wako kwa whatsapp hiyo hapo juu.**

***Ilipoishia…***

**“Tumemuua mmoja!” Alisema kiongozi wao. “ Na huyu mwingine tutamtisha kwa njia moja ama nyingine, hatathubutu tena kutuibia chochote hapa!!”. Alinyanyua upanga wake juu hewani huku akitoka nje ya pango.**

***Endelea...***

“Chukua hii maiti ya huyu jamaa mkaining’inize juu ndani ya pango!!” Alisema kiongozi wao. “Mwili wake utakuwa ni onyo kwa yeyote atayekuja humu ndani!”. Ilikuwa inatisha sana.

Hivyo basi, wezi wakachukua kamba na kuuning’iniza mwili wa Kassim juu ndani ya pango na kisha wakatoka kulekea kwenye farasi wao tayari kwa safari ya kwenda mjini tena kuiba.

“Pango letu limeshakaribia kujaa dhahabu” Alisema kiongozi wao. “Na muda si mrefu tutapata nyingine zaidi!”. Baada ya kusema hayo wakaondoka zao wote.

Siku nzima mke wa Kassim alikaa dirishani akimsubiria mumewe atoke huko pangoni. “Uko wapi Kassim?” alijisemea mwenyewe,”Uko wapi?, kwanini usingebaki na mimi huku? Kwanini ulienda pangoni kutafuta dhahabu?” yote haya alijisemea ingawa hajui kilichotokea huko pangoni.

Mpaka jua lilipozama, mke wa Kassim akaona sasa si muda wa kukaa na kusubiri, lazima kutakuwa na tatizo tu. Akakimbia haraka kwa Alibaba na kugonga mlango.

Alibaba alipofungua tu, aliingia ndani na kuanza kulia. “Alibaba nisaidie, kaka yako tangu alipoondoka asubuhi leo hajarudi mpaka sasa hivi kutoka pangoni! Aliondoka kabla jua halijachomoza vizuri na punda kumi, aliniambia anaenda huko kuchukua dhahabu, nilikaa dirishani kumsubiria siku nzima, nadhani kuna jambo baya limemtokea huko, tafadhali nisaidie, Alibaba! Tutafanya nini?”

“Usihofu,” alijibu Alibaba, “Nitakwenda na punda huko msituni kumtafuta. Nenda nyumbani na unisubirie, nitarudi muda sio mrefu na nakuahidi kwamba nitakuja na kaka yangu.”

Hivyo basi Alibaba alichukua pun-



da wake watatu na kuelekea msituni. Wakati anaendelea kwenda msituni, Alibaba alikuwa akimtafuta kwenye miti miti huku akiita jina lake, lakini hakuona wala kumsikia mtu yeyote. “simpati Kassim, wala punda wake kumi pia siwaoni” Alibaba alijisemea. “Kassim aliweza kujua lile pango lilipo? Je aliweza kupata dhahabu? Mh! Huenda mkewe akawa yuko sahihi labda mumewe kuna jambo baya limemtokea.”

Alibaba alipokaribia pangoni, aliona michirizi ya damu ardhini. “hii ni ishara mbaya!” alifikiria. Kisha akasema, “nitaenda pangoni nikaangalie kama Kassim yupo mle ndani”. Aliwaacha punda wake watatu chini ya mti kisha akasogea mpaka karibu na lango la pangoni kisha akasema lile neno la siri, “Fungukaaaa sesmiiiii!!!”

Lango lilipokuwa likifunguka taratibu, Alibaba aliona kitu chenye kushtua sana. Aliona mwili wa mtu ukining’inia juu ya pango, alipokaribia kuutazama kwa karibu zaidi akaona kuwa ni kaka yake, Kassim. Alibaba alianguka chini kwa magoti na kuanza kulia. “Masikini Kassim!!” alisema! “alikuwa ni mwenye tamaa, lakini ni kaka yangu. Ona sasa kundi la wezi limemuua kwasababu ya tamaa!!”

Aliendа ndani ya pango zaidi na kupata dhahabu zilizofungwa na nguo kubwa nyeupe. Alizitoa dhahabu zile na kuchukua ile nguo kubwa kisha akaufunga mwili wa kaka yake latika nguo ile, kisha akaubeba mwili wa kaka yake mpaka kwenye punda mmoja kati ya wale watatu aliokuja nao. Kisha akaufunika mwili ule na baadhi ya kuni ili usionekane na watu njiani. Alibaba hakutaka watu wajue kuhusu hazina zile ndani ya pamoja na wezi 40. Kisha akarudi ndani ya pango.

“Nitachukua kiasi kidogo cha dhahabu zaidi,” alisema Alibaba, “kiasi cha kujaza makapu manne niliyokuja nayo na wale punda wangu.”

Alijaza dhahabu kwa punda wawili kisha akazifunika na kuni kisha akasema neno la siri la kufungia pango, “Fungaaaaa sesmiii!!!” na kisha akaondoka.

*ITAENDELEA...*

**Ameandika Mwafrika Merinyo**

Ni usemi wa Kiingereza, chambilecho *"Don't judge a book by its cover"*. Kwa usemi huu tunaaswa kuwa na hadhari ya kupitisha hukumu juu ya mtu au mazingira fulani kabla hatujayachungua au kuyajua vema. Nilipokuwa safarini kutoka Lindi kuja Dar es Salaam jana, niliona mtandaoni tangazo lililotolewa na Mtoto wa Beka almaaruf Tungo Tata Kingdom kwamba angezindua duka la vitabu maeneo ya Manzese jijini Dar es Salaam. Mara moja niliamua nimtembelee Mtoto wa Beka katika tukio lake hili. Nilisukumwa na mambo mawili katika kufikia uamuzi huu, na mambo haya ndiyo kiini cha tafakari yangu ya leo.

Jambo la kwanza lamhusu Mtoto wa Beka mwenyewe. Nilimfahamu huyu kutokana na ukurasa wake wa *Facebook* ambao awali akiuita Tungo Tata na baadae kuurasimisha zaidi kuwa Tungo Tata Kingdom.

Ni mbinu ya kutibua mazoea ili kuwaamsha hadhira kutazama kulikoni. Na katika mtibuo huo Mtoto wa Beka ndipo anapochomeka ujumbe au falsafa zake ambazo ni nzito si haba.
Baada ya kusoma machapisho yake kadhaa, nilimaizi kwamba huyu si mwandishi wa kupuuza, anayo mambo mazito anayotaka kuyafikisha kwa jamii. Yeye binafsi anadai kwamba uandishi wake unalenga kuwavutia na kuwahamasisha wasomaji ambao huchoshwa na uandishi wa kimazoea, au tuuitao "wa kistaarabu". Mtoto wa Beka anadai kwamba uandishi wake utaziba ombwe ambalo ameliona, ambapo wasomaji wa uswazi wamekuwa wakikosa uandishi unaoendana na ladha halisi ya maisha na mazingira yao.

Jambo la pili ni mshawasha wa kutaka kuona duka lake la vitabu aliloamua kulianzisha "uswazi". Tumezoea kuona maduka ya vitabu maeneo ya Oysterbay, Masaki, Mtaa wa Samora kwenye maduka makubwa au *'shopping malls'*

# TAFAKARI YA MWAFRIKA

Niliposoma mashairi yake kwa mara ya kwanza, yalinishtua, yakanikosesha utulivu.
Niliwahi kumwambia:

***"Hongera sana gwiji wa tungo tata! Nadhani utata wako ndio unaokupambanua na watunzi wengine. Kuna wakati unanifurahisha na kuna wakati unanikera, hasa unapokosa tasfida (labda unafanya kusudi au umelenga wasomaji wa aina fulani!) Kuna wakati natamani nisisome mashairi yako, lakini najiambia "labda leo hataharibu sana, ana kitu huyu, acha nisome tu!" Una uwezo mkubwa wa kuongea mambo mazito kwa namna ya kipuuzi sana, kama mlevi vile (si unajua akishautwika haogopi kuropoka?) . . ."***

Mtoto wa Beka huandika kwa mtindo wa kushtua, hutumia lugha tata na aghalabu yenye semi kali au maneno ambayo hayajazoeleka kwa mitindo ya uandishi tunaoweza kuuita "staarabu". Katika mazungumzo niliyofanya naye leo tukiwa tumekaa kwenye mgahawa mdogo tukinywa maziwa na kuteremshia keki kutoka dukani kwa mangi mmoja, nimemaizi kwamba matumizi yake ya lugha ni ya makusudi, ni mtindo kama ule wautumiao wasanii wa Bongo Fleva wa "kuchana".

na maeneo kama ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mtoto wa Beka, au mtata wa fasihi, anafanya mapinduzi ya kupeleka fasihi kwa 'watu'.

Nilipofika hapo Mzambarauni, eneo kati ya Manzese na Mburahati, nilimkuta akihangaika kupaweka sawa mahali ambapo anapaandaa kuwa duka jipya la vitabu vya aina mbalimbali. Ametoa mwito kwa waandishi wengine wa vitabu wanaoishi Dar es Salaam kuunga mkono katika jitihada zake za kuwapelekea watu fasihi mtaani kwa kupeleka vitabu dukani kwake ambako atavifanyia utangazaji au promo bure na kuanza kuviuza kuanzia Jumamosi ya tarehe 27 Januari, 2024.

Namuombea kila la heri gwiji wa tungo tata,
Mtoto wa Beka!

Mwafrika Merinyo ni mmoja wa waandishi nguli hapa nchini. Ameandika riwaya kadhaa pia ni mwandishi wa mashairi. Isitoshe pia ni mbunifu wa mitindo.

Kama haukuwa ukijua, usikiapo *'Sinza Afrika Sana'* basi tambua kuwa jina la mahali hapo limetokana na nguli huyu. Apewe maua yake!

# SHUBAKA LA VITABU

**Katika Safu yetu ya SHUBAKA LA VITABU leo tutawaletea Maktaba kumi (10) bora duniani. Je; wazijua hizo. Karibu uwe nasi upate kujua haya,**

7. MAKTABA YA JAPAN (NDL) NATIONAL DIET LIBRARY

Hii ni Maktaba ya Taifa ya Japan ni namba saba (7) katika ya maktaba kubwa duniani kadiri ya mtandao wa Wikipedia. Ilianzishwa mwaka 1948 kwa lengo la kuwasaidia wanachama wa NDL (Kokkai) katika tafiti za sera za umma.

Nation Diet Library imegawanyika sehemu mbalimbali. Lakini shughuli zake kubwa zinafanyika katika kituo cha Tokyo na Kyoto halafu kuna matawi sehemu nyingine nyingi.

Maktaba hii ya Japan ni muunganiko wa maktaba tatu zilizosambaratika; Maktaba ya House of Peers, House of Representatives na Imperial Diet. Majengo yake yamesanifiwa na Maekawa Associates, architects and Engenering kampuni ya huko Japani.

Mpaka mwaka 2016 ilikuwa na items 41,881,649 kaatika hivyo vyote kulijumuisha vitabu, majarida, magazeti, makala za kielektroniki, maandiko ghafi, machapisho ya kiofisi, ramani, miziki na vingine vingi. Bajeti yake inakadiriwa kuwa ni Yeni za Kijapani Milioni 20,163. ina waajiriwa 908.



8. MAKTABA YA TAIFA YA UJERUMANI (GERMAN NATIONAL LIBRARY 'DNB')

Hii ni miongobni mwa maktaba kubwa duniani. Katika mtiririko ndani ya Wikipedia, inashika nafasi ya nane. Ilianzishwa mwaka 1912 na inapatikana katika Jiji la Frankfurt na Leipzig.

Katika maktaba hii kuna hifadhi ya items Milioni 43.7 mpaka kufikia mwaka 2021. katika hizo kuna nyaraka za kawaida, rekodi za sauti, machapisho ya kidijitali, machapisho ya mtandao, vitabu, ramani, magazeti na makala nyingine nyingi.

Kila makala iliyochapwa kwa lugha ya Kijerumani imehifadhiwa humu, na kila makala iliyoandikwa na Mjerumani imehifadhiwa humu na kila makala iliyoandikwa kuhusu Ujerumani imehifadhiwa humu.

Bajeti yake ni Euro Milioni 54.9 kufikia mwaka 2018. na ina waajiriwa 641.



**Anna Mbise Mobile Library**
**Kitabu:** *I can, I must, I will*
**Mwandishi:** Reginald A. Mengi
**Msomaji:** Paul Makuri
**Mkoa:** Dodoma

Niliyojifunza kutoka kwenye kitabu hiki:-

**1. Mchango wa malezi na familia katika mafanikio:** Mzee Mengi anaanza kwa kukumbuka namna familia yake ya maisha ya kawaida ilivyowakuza yeye na ndugu zake katika maisha ya maadili na kuwafunza kufanya kazi kwa bidii na kusaidia wahitaji. Hadi anafikia kwenye kilele cha mafanikio bado alikuwa akikumbuka yale malezi mema toka kwa wazazi wake na hakuacha kusaidia wahitaji na kufanya kazi kwa bidii.

**2. Mafanikio katikati ya Changamoto:** Mzee Mengi anaelezea alivyopata nafasi kwenda kusoma Uk. kwa kusitisha masomo yake ya kidato cha tano na sita. Lengo tu apate fursa ya kuwa mhasibu, asipoteze fursa ya kwenda Ulaya na kutimiza ndoto yake. Pamoja na changamoto alizopitia hakukata tamaa, alipigania ndoto yake hadi akaitimiza na kufanikiwa kuwa *Chartered Accountant- - ACCA*. Ilikuwa kama ndoto ngumu kwa kipindi hicho, lakini aliitimiza. Lakini pia hata mafanikio yake mengi katika biashara aliyapata pindi nchi ilipokuwa kwenye mdororo wa uchumi. Alipambana kupata bidhaa adimu kwake aliitumia kama fursa, na kutafuta bidhaa muhimu na kuziingiza sokoni.

**3. Mafanikio ni pamoja na kuwa tayari kujitoa Sadaka:** Mzee Mengi ali-*risk* hadi maisha yake ili tu atimize ndoto zake. Kuna kipindi wenzake walikuwa wakimshangaa kwa nini hataki kuajiriwa serikalini huku kuna fursa nyingi za kupata nafasi kubwa ila anahangaika kwenye *private sector* isiyokuwa na uhakika wa kesho. Lakini sio mzalendo kwa kutofanya kazi serikalini. Yeye alitazama zaidi kesho yake na mafanikio aliyokuwa amelenga kuyafikia. Hata hivyo mara nyingi hakupendwa na washindani wake kibiashara hasa kwa yeye kuwa mwafrika/ngozi nyeusi, ambao hawakuwa wamiliki uchumi kipindi hicho. Hata viongozi wa serikali mara nyingi walitofautiana naye kwa sababu alitazama mambo kibiashara zaidi na kwa mapama ya kesho.

**4. Uzalendo kwa Taifa lako si lazima uwe muunga mkono wa Watawala tu:** Tangu mwanzo hadi mwisho wa maisha ya mafanikio yake, Mzee Mengi alikuwa *critics*, alionekana mpinzani na mkosoaji. Lakini mapambano yake yalilenga kusaidia na kuinua hali ya Mtanzania wa kawaida na kubadili sera kandamizi. Alifanikiwa sana hadi kupewa tuzo mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa kuwa mstari wa mbele kupigania haki za wasiokuwa na sauti.

**5. Moyo wa kujitoa na kusaidia:** Mzee Mengi anaeleza alivyorithi moyo wa kujitoa toka kwa mama yake mzazi na kaka yake mchapakazi. Pamoja na kusaidia na kujitoa sana kwa jamii hakuwahi kupungukiwa zaidi alizidi kufanikiwa na kupata hadi ziada.

**6. Ndoto na dhamira zetu zitusukume ktk kufikia mafanikio yetu:** *Yes I can, I must, I will; the spirit of success* . Hatupaswi kuwa na *excuse* yotote katika kupigania ndoto na dhamira zetu. Katikati ya sera ngumu, sheria kandamizi, jamii isiyotuunga mkono nk, dhamira zetu njema zituongoze kufikia mafanikio yetu tena ya juu.

**7. Tupende na kulinda familia zetu:** Mzee Mengi anaonesha namna familia ilivyokuwa nguzo muhimu katika kufikia mafanikio yake binafsi, malezi toka kwa wazazi wake, kaka yake alivyomfadhili pale alipokwama malipo ya ada masomoni UK. Alivyokuwa tayari kulinda na kupigania familia yake binafsi na hata alivyoumia sana baada ya kifo cha kijana wake aliyempenda sana.

**8. Bidii na Nidhamu katika kazi.** Mzee Mengi anaiasa jamii hususani vijana, kuwa hakuna mafanikio rahisi, wala ya mkato katika kufikia mafanikio binafsi. Ni lazima kujituma, kutumia vizuri kila fursa inayojitokeza. Kufanya kazi kwa bidii na kutobaki watazamaji na walalamishi badala ya kuchukua hatua. Uthubutu katika maisha ndiyo huleta mafanikio. Wakati ni sasa sio kesho.

Asanteni.

Read & Write
With
Anna Mbise




TANGAZA na NGURUMO YA MWANDISHI kwa bei nafuu na ya kirafiki.
Matangazo madogo ni Tsh 5000@ na Tangazo la kurasa nzima ni Tsh 10000@.
Wasiliana nasi kwa simu *(call & Whatsapp)* 0766974865 na Email: jamvilasimulizi@gmail.com

## UTAMU WA CHAI SUKARI

Utamu wa chai sukari, majani chai kwa mbali
Utamu wa chai sukari, shuti unywe na futali
Utamu wa chai sukari, nani asiyeijali?

Utamu wa chai sukari, maji shuti yawe moto
Utamu wa chai sukari, weka mbali na mtoto
Utamu wa chai sukari, tunapitia msoto

Utamu wa chai sukari, mbona mwatubania
Utamu wa chai sukari, viwanda mwatufungia
Utamu wa chai sukari, bei mwatupandishia

Utamu wa chai sukari, watoto huku wanalia
Utamu wa chai sukari, hatuelewi kadhia
Utamu wa chai sukari, kwani miwa meishia?

Utamu wa chai sukari, hata mama unajua
Utamu wa chai sukari, nani anayezingua?
Utamu wa chai sukari, mbinu chafu gundua

Utamu wa chai sukari, maisha yarudi nyuma
Utamu wa chai sukari, ladha yetu mwatunyima
Utamu wa chai sukari, tuoneeni huruma

Utamu wa chai sukari, bidhaa mepanda bei
Utamu wa chai sukari, kamwe hamtutetei
Utamu wa chai sukari, zalisho hutembelei

Utamu wa chai sukari, hebu tuambieni ukweli
Utamu wa chai sukari, bei mepaa kweli
Utamu wa chai sukari, viwanda havizalishi kweli?

Utamu wa chai sukari, 84' twarudi
Utamu wa chai sukari, ulanguzi litaradadi
Utamu wa chai sukari, naona kule twarudi

Utamu wa chai sukari, waweza itia chumvi?
Utamu wa chai sukari, au tunywe hivihivi?
Utamu wa chai sukari, mbona mwatufanya hivi?

**Shujaa Maneno**
**Minde — Bagamoyo Pwani**

## WAAMBIE WANYAMAZE

Wape Salamu Malenga, Watusemao Vibaya
Waache Kuchonga Ngenga, Kama Wanaona Haya
Wapunguze Ushambenga, Watungamane Kwa Kaya
Watusemao Pembeni! Waambie Wanyamaze

Watusemao Pembeni, Peleka Salamu Zao
Waambie Nyamazeni, Tungo hizi si za Kwao
Wenyeji Sio Wageni, Sisi Sio kama Wao
Watusengenyao Chonjo! Waambie Wanyamaze

Watusengenyao Chonjo, Wambie Tumesikia
Wasiukuze Uongo, Tukaja Kuwachukia
Wapanguse Tongotongo, Waione Yetu Nia
Wasijione Wajuzi! Waambie Wanyamaze

Wasijione Wajuzi, Mashairi si Udini
Waambie Wadakuzi, Wajishike Akilini
Hatujazianza Juzi, Hizi Tungo ni Makini
Tutaja Kuwalipua! Waambie Wanyamaze

Tutaja Kuwalipua, Waambie Wasichonge
Tayari Tushawajua, Kumbe Wanaona Donge
Vile Tunavyotumbua, Majipu sio Kinyonge
Kama Hawawezi Tungo! Waambie Wanyamaze

Kama Hawawezi Tungo, Waseme Tuwafundishe
Wasiumwage Utumbo, Maneno Mavi Yaishe
Tumewafumbia Fumbo, Majibu Wasahihishe
Kwakuwa Tunawapenda! Waambie Wanyamaze

***Tungo Tata Kingdom***

***+255 693 246 041***

***Mwaka wa Mashairi***

**Unaweza kuchangia chochote ili kuwezesha jarida hili kuwa bora na kuwafikia wengi zaidi. Kama upo tayari, changia kiasi chochote kupitia MPESA LIPA NAMBA 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Na Mungu atakujazi.**

# Habari Picha

Usiache kutembelea duka jipya la vitabu la Tungo Tata Kingdom lililopo 'Kitaa' huko MANZESE ujipatie vitabu mbalimbali vya waandishi mbalimbali.

Au kwa uhakika zaidi wasiliana na Mtoto wa Beka kwa simu namba 0693 246 041



Baadhi ya walioshuhudia kuzinduliwa kwa duka jipya la vitbu la Tungo Tata Kingdom, katika picha ya pamoja.

**Siku ya ufunguzi wa Duka la vitabu la Tungo Tata Kingdom (27/1/024). Mwafrika Merinyo akiteta jambo na Molito Brand.** ***Kalamu ivunjavyo tabaka la rika***






Kushoto ni Mwafrika Merinyo akimkabidhi Hussein Beka Mwinshehe kitabu cha 'WATOTO WA MJINI' alichokitunga na kukiandika yeye mwenyewe. Picha hii ilipigwa siku alipomtembelea huko Manzese.

**Ukilipata jarida hili, mtumie na mwezako.**

**"Tuambukizane furaha kwakuwa siyo ugonjwa"**
**by Luvanda Vitenge**

**'VITUKO VYA UHURU' - Harakati za kupigania Uhuru wa Tanganyika na vituko vyake. Ni kitabu kilichoandikwa na M.W. Kanyama Chiume—1973. Hii ni Kutoka Maktaba**

**2. WATOSWA MTONI**

TANU iliingia kwa mbinu za hali ya juu katika wilaya ya Ulanga. Huko, wakoloni waliwafanya wananchi wapigane wao kwa wao, ama wao na watemi wao. Kwa propaganda kali waliwapumbaza machifu kuamini kwamba TANU kingeleta vu=ita vya Maji Maji nchini.

Huko Ifakara, kila kulipokucha, lilikuwa jambo la kawaida kwa wana-TANU kuona maneno ya vitisho yameandikwa milangoni pao katika lugha ya Kiarabu, ama dondoo kutoka Korani Tukufu. TANU ilipigwa marufuku Kiberege na viongozi kadhaa walitiwa mbaroni na kupelekwa jela Mahenge. Siku moja, mmoja wao, yaani ndugu Ramadhani Kondo, aliwakuta polisi wanapekua nyumba yake. Polisi eti waligundua pembe za ndovu zilizokuwa zimefukiwa uani! Akakamatwa na kushtakiwa kwa kuwa na pemba hizo bila kibali. Aliponea chupu chupu kwenda jela, lakini mwenzake Ndugu Mohamed Paza, hakuwa na bahati, akafungwa, kwa mashtaka kama hayo.

Kivumbi hasa kilikuwa Malinyi na Utengule. Sehemu hii ilitawaliwa na Chifu Towagale, mmoja wa machifu wakubwa katika wilaya ya Ulanga. Ili awapende na kwahiyo awe upande wao, wakoloni waliomjengea Chifu huyo jumba kubwa la orofa kutokana, inavyosemekana, na michango ya wananchi na fedha za mishahara ambayo haikulipwa! Katika hali hiyo, Chifu huyo alioa wake themanini, kila mmoja akijiona mkubwa kwa upande wake. Mkuu wa wilaya, D.C Scott na baadaye Berkeley, walifanya kila njia kumtenganisha na watu wake ikiwa ni njama ya kuzuia TANU isienee katika wilaya ya Ulanga. Mwanaye, Karim, alitawala Malinyi kama chifu mdogo.

Sehemu hizo zote mbili zilikuwa na mzozo mkubwa sana kati ya Wabena (watawala) na Wandamba (wenyeji). Wandamba walidai kwamba wao ndiyo wangekuwa watawala. Na katika mzozo huo, Ndugu Almasi Mkabila, mkuu wa Wandamba, aliuawa na mwili wake ulitupwa majini.

Kutokana na kitendo hicho Binti Njaramoto na mabwana Antoni Ngwale, Joni Kawelewele na Taibu Makelo, wakaamua kwenda Dar es salaam kuingia TANU wakiwa na matumaini kwamba TANU ingewasaidia katika madai yao ya uchifu. Walipokuwa Dar es salaam walishauriwa na wana-TANU, miongoni mwao akiwemo Ndugu Faraji Ali Kilumanga, kujiunga na wenzao nchini kudai uhuru wa nchi nzima na sio utawala wa Undamba tu. Baada ya kupelekwa kwa Ndugu Dosa Aziz, Makao Makuu ya TANU, walikata kadi na kuonana na Mwalimu Nyerere tarehe 8 Julai, 1956.

Mara tu baada ya tukio hilo, Mwalimu alimtuma ndugu Vincent Mponji akiwa Katibu wa TANU wa Jimbo la Mashariki, kufuatana nao hadi Mahenge kufungua tawi la TANU kama wajumbe hao walivyoomba. Huko mambo hayakuwa mepesi. Mkuu wa Wilaya alikataa kabisa kumruhusu Ndugu Mponji kufanya mkutano Malinyi ama Utengule. Hivyo Ndugu Mponji alirejea Dar es salaam, akiwa ameacha kadi kwa mwalimu Cosmas Ntanga na akiwa na matumaini kwamba mwenzake angerudi kujaribu tena.

Wale vijana walipoona kuwa hakurudi kujaribu tena, wakafunga safari kwenda Dar es salaam kuonana tena na Mwalimu Nyerere. Safari hii Mwalimu aliwapa barua kwa Ndugu Lira Mwinyikondo, Mwenyekiti wa TANU Jimbo la Mashariki, kumwomba aende Mahenge yeye mwenyewe.

Mwenyekiti huyo, akifuatana na Ndugu Mohamed Juma, katibu wa TANU Wilaya ya Kilosa, waliondoka kwa miguu mara moja, hapa na pale wakidowea malori.

"Lakini kila tulipopita," alisema Ndugu Lira, "tulikuwa kama tunanuka kwani wakati huo TANU ilikuwa inaogofya sana."

Walipochukua nafasi ya kuwahutubia juu ya TANU wananchi waliokusanyika kuezeka soko lao la Kidatu, wote waliokusanyika kuwasikiliza walichukuliwa papo hapo kwenda jela miezi mitatu pamoja na chifu wa hapo. Mwenyeji wao Ndugu Abdala Ali, alifungwa miezi sita. Chifu Mtoahanje wa Kiberege, alikataa kabisa kuingilia uamuzi wa chifu wake mdogo ili kuwaacha huru watu hao.

***Usikose sehemu ya 4***

# HAKUNA MWANAFUNZI ANAYEPENDA KUFELI—2

Mwl. Juliana Isondo.
Soni Day Secondary



Karibuni sana katika mwendelezo wa makala iliyopita. Katika makala hii tunaangazia mambo Muhimu ya kumsaidia mwanafunzi kufanya vizuri darasani;

**Fikra/mawazo:** Matokeo ya mwanafunzi yeyote yule yapo kichwani mwake. Muulize mwanao/wanafunzi, muda mwingi wanafikiri ama wanawaza nini? Wanafunzi wanaofanya vizuri maranyingi huwa wanafikiria namna gani wanaweza kuboresha matokeo yao.

**Mtazamo:** Jambo jingine linaloleta matokeo mazuri ni mtazamo. Mwanafunzi anayelalamikia kuwa somo fulani gumu mara nyingi huwa haweki jitihada na mikakati ya kufanya vizuri. Mwanafunzi mmoja tumwite Juma, alihamia shule ambayo haifundishi masomo ya uchumi, na yeye alikuwa anaamini kuwa uchumi ni maisha yake, sio somo tu. Walimu na wazazi wake walimshauri kuacha kusoma uchumi lakini yeye alikataa, aliendelea kujisomea mwenyewe, alitafuta maswali, wakati wa likizo alisoma *tution*, alikutana na wenzake wanaofundishwa na walimu wakawa wanasoma pamoja na mwisho wa siku alifanya vizuri zaidi ya waliokuwa na walimu wa kutosha.

**Kusoma vitabu:** Wazazi wekezeni katika vitabu na muwahimize watoto kusoma vitabu mnavyowanunulia. Kama nilivyosema kwenye makala iliyopita kuwa kuna wanafunzi wanaoweza kujiongoza na kujisimamia wao wenyewe na mambo yao yakaenda bila shida pia wapo wanafunzi ambao wanasoma vitabu bila kulazimishwa na mtu yeyote. Ni jukumu lako mzazi kujenga utamaduni wa kuwasimamia watoto wako kujisomea bila kulazimishwa wala kusimamiwa.

**Nidhamu:** Pamoja ya kuwa kusoma ni muhimu lakini kusoma bila kuwa na nidhamu ni kazi bure. Mwanafunzi yeyote yule anatakiwa kuwa na nidhamu, ajiheshimu yeye mwenyewe, awaheshimu walimu, wenzake na jamii nzima inayomzunguka.

**Malengo:** Kila mwanafunzi anapaswa kuwa na malengo binafsi, anatakiwa kusimamia malengo yake mpaka yaweze kutimia bila kukatishwa tamaa na mtu yeyote. Wazazi na walimu msiwe wakatisha tamaa, mwanafunzi anapokushirikisha malengo yake amekuamini na anahitaji msaada hivyo ni vyema umtie moyo na uwe chanzo cha yeye kufanya vizuri.

**Kuwafundisha wengine:** Hii ni njia muhimu sana, na inaweza kufanyika kwa namna tofauti tofauti. Mfano nyumbani mwanafunzi X anaweza akawa anawafundisha wanafamilia kitu alichofundishwa shuleni siku hiyo au anawafundisha wanafunzi wenzake. Kuwafundisha wenzake ni vizuri zaidi maana wanakuwa wanamfuatilia kujua kama ameelewa kile alichofundishwa au hajaelewa.

**Kuelewa na kukariri:** Walimu wengi huwa wanapinga mbinu ya kukariri, ninaamini kuwa mwanafunzi yeyote anayetaka kufanya vizuri ni lazima aelewe kisha akariri alichokisoma. Hapa mzazi unaweza kumsimamia mwanao asome kitu fulani kisha akupatie daftari alafu yeye aseme kwa kichwa kile alichokisoma. Hata mwanafunzi mwenyewe anaweza kutumia mbinu ya karatasi kujisomea mwenyewe, anasoma

# ELIMU JAMII:

kisha anafunika daftari na kuanza kuandika alichokisoma.

**Kuhudhuria na kufuatilia kipindi:** Mwanafunzi anayehudhuria kipindi na kukifuatilia unaweza ukamwekea dhamana kuwa atafanya vizuri katika mitihani yake. Ni muhimu sana kwa mwanafunzi kuhudhuria vipindi.

**Hamasa:** Kuna wakati hamasa ya kujisomea inaweza kuisha, mwanafunzi akakosa hamu ya kujisomea kabisa, hapa sasa ni jukumu la mzazi kumuonesha kuwa anapaswa kutumia nidhamu. Nidhamu ni kufanya jambo fulani uwe unajisikia ama haujisikii. Ni lazima kujilazimisha kusoma hatakama hajiskii.

**Mwongozo wa maisha:** Mzazi hili haliepukiki. Mara kwa mara msaidie mwanao kwa kumwonesha njia sahihi ya yeye kuenenda. Mzazi mmoja alikuwa anasumbuliwa sana na mtoto wake. Kuna wakati alikata tamaa kabisa ya kuendelea kumwelekeza. Tulipozungumza nilimsisitiza asiache kumwelekeza. Juzijuzi alinifuata na kunishukuru maana mtoto wake alishabadilika kabisa.

**Kuwa king'ang'anizi:** Hii njia huwa maranyingi nawafundisha wanafunzi wengi ninapopita mashuleni. Hapa mwanafunzi hapaswi kutulia mpaka atakapoona anafanya vizuri, anapaswa kusoma na kusoma na kuendelea kusoma mpaka matokeo yatakapo badilika.

**Kubadili mbinu za usomaji:** Mwanafunzi ajitahidi kubadili mbinu za usomaji mpaka atakapopata mbinu inayoendana kabisa na yeye. Mbinu za usomaji zipo nyingi sana kuna ya kusoma mwenyewe au kusoma katika kundi. Mwanafunzi mmoja tumwite Maria alinifuata baada ya kupokea mitihani yake yenye alama D, akaniaomba nimsaidie ili atoke kwenye hizo alama basi nikamshauri atafute mwenzake/wenzake wa kusoma nao basi wakaanza kusoma. Mitihani iliyofuata akawa angalau alama zilianza kubadilika ukilinganisha na mwanzo.

**Kuusikiliza mwili:** Mwanafunzi asilazimishe kabisa kusoma mwili ukiwa umechoka. Anapaswa kupumzika kwanza kisha aendelee baada ya muda, wengi hudhani kupumzika ni kupoteza muda. Si kweli kupumzika ni kama kuweka simu kwenye chaji ukiamka unaikuta imejaa vizuri na inakuwa na nguvu ya kufanya kazi zaidi.

**Kushiriki katika shughuli zisizo za darasani:** Wanafunzi wengi wanaepuka kushiriki katika michezo. Wanaamini kuwa kushiriki katika michezo ni kupoteza muda. Michezo/mashindano yoyote ni muhimu kwa mwanafunzi kwasababu inamsaidia kuimarisha mwili na akili lakini pia inakuza urafiki na  mwisho michezo ni ajira. Mwanafunzi ashiriki katika michezo bila kuacha na wazazi msiwakataze watoto wenu kujiunga katika vilabu vilivyopo mashuleni.

**Kujali muda:** Muda uliopangwa katika ratiba ikitokea ukafuatwa vizuri mwanafunzi ana uwezo wa kufanya vizuri bila kipingamizi chochote. Iko hivi wanafunzi wengi hupoteza muda wao muhimu kwa kupiga soga ama kucheza. Hii inawapelekea kujilimbikizia mambo mengi ya kusoma na kufanya siku za mitihani kuwa siku ngumu, wanafunzi wajenge desturi ya kutumia muda vizuri siku zote.

Asante sana kwa kuwa name **Naitwa Juliana Isondo**

Mwalimu kutoka Bumbuli Tanga

Usiache kunifuatilia katika kurasa zangu

**Facebook na Instagram**

# Tangazo




www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI


Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi
jamvilasimulizi@gmail.com